

Maelezo kuhusu hatua za somo

Ili kufikia azma ya ufundishaji na ujifunzaji unaolenga kufanya mwanafunzi kuwa kiini cha ujifunzaji katika kujijengea maarifa, stadi na mielekeo chanya, hatua za ufundishaji na ujifunzaji katika andalio hili zimebainishwa kwa kufuata hatua 4 ambazo ni utangulizi, Kuendeleza ujenzi wa umahiri, Kubuni, na Tathimini.

Utangulizi

Sehemu hii inalenga kumtambulisha mwanafunzi katika ujenzi wa umahiri uliokusudiwa. Katika hatua hii, mwalimu anatarajiwa kuwasaidia wanafunzi kuhodhi kipindi kwa kutumia shughuli mbalimbali kama vile kujadili namna kile watakachojifunza kilivyo na muhimu katika maisha yao, namna wamekuwa wakitumia maarifa wanayotarajia kujifunza bila wao kujua, kuimba, kucheza, na shughuli nyingine kama hizo. Kwa ufupi, hatua hii inatambua kuwa mwanafunzi siyo tabularasa, kwamba hata maarifa yakiwa mapya kiasi gani, bado ana nafasi ya kushirikisha chochote anachokifamu kuhusu anachotarajia kujifunza. Hivyo, ni muhimu mwalimu akahakikisha shughuli katika utangulizi zinaakisi maarifa mapya ambayo mwanafunzi anatarajia kujijengea.

Kuendeleza ujenzi wa umahiri

Hatua hii ina uhusiano mkubwa na utangulizi, ambapo mwanafunzi anatarajiwa kufanya shughuli zinazolenga kuendeleza kile alichoonesha anakifahamu kuhusu umahiri mpya anaotarajia kujifunza. Katika hatua hii, mpe mwanafunzi shughuli mbalimbali zinazompeleka kwenye kujenga uelewa kwa kupitia maandiko, kutazama video, kufanya majadiliano, kudadisi, kuchunguza, hojaji, na shughuli zingine kama hizi. Kwa kadiri inavyowezekana, wape wanafunzi fursa ya kuwasilisha waliyojifunza na uwape nafasi ya kutolea ufafanuzi kuhusu yale waliyojifunza na wanayoyaamini.

Kubuni

Kwa kawaida, mwanafunzi akishajenga uelewa wa umahiri uliokusudiwa, anakuwa katika nafasi ya kuweza kuutumia katika miktadha mbalimbali. Kwa mfano, mwanafunzi anaweza kuchora picha au kusimulia hadithi kulingana na umahiri husika. Hivyo, katika kipengele hiki, waongoze wanafunzi kufanya shughuli zinazolenga kuhuisha au kutumia maarifa waliyojifunza katika kutatua changamoto halisi katika maisha.

Tathmini

Tathmini ni kipengele muhimu katika mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji. Hivyo, wape wanafunzi shughuli zinazolenga kuwapa fursa ya kujitathmini na kutathminiana ili kubaini utofauti kati ya kiwango chao cha awali cha uelewa na baada ya kujifunza. Hivyo, walimu wanahamasishwa kutumia njia mbalimbali za upimaji kama vile mkoba wa kazi, hojaji, kuandaa vitu halisi, mazoezi, mitihani na mbinu nyingine nyingi za upimaji. Walimu wana wajibu wa kuwafuatilia na kuwasaidia wanafunzi kupitia shughuli za upimaji ili kubaini kiwango cha ujifunzaji kabla na baada ya kujifunza maarifa mapya.

Mwisho, mwalimu unashauriwa kuelewa kikamilifu matakwa ya kila hatua na kusimamia utekelezaji wake. Ni matumaini ya TET kuwa utekelezaji wa namna hii wa ufundishaji na ujifunzaji utawawezesha wanafunzi kukuza maarifa, ujuzi na mielekeo chanya na hivyo kuwa na umahiri na

stadi muhimu katika karne ya 21 zitakazowasaidia katika kumudu maisha yao ikiwemo kujiajiri na kuajirika.

Jina la Shule: **Jina la Mwalimu:**

Darasa: **Tarehe:**

Muda:

Somo:

Idadi ya Wanafunzi					
Waliosajiliwa			Waliohudhuria		
Wasichana	Wavulana	Jumla	Wasichana	Wavulana	Jumla

Umahiri Mkuu:

Umahiri Mahususi:

.....

Shughuli Kuu:

.....

Shughuli Mahususi:

.....

Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji:

.....

Rejea:

.....

.....

.....

Mchakato wa Ufundishaji na Ujifunzaji

Hatua	Muda (Dakika)	Shughuli za Ufundishaji	Shughuli za Ujifunzaji	Vigezo vya Upimaji
Utangulizi				
Kuendeleza ujenzi wa umahiri				
Kubuni				
Tathimini				

Maoni:.....

